

Uchanganuzi wa Makosa ya Kimofofonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kitachoni Wanapojifunza Kiswahili kama Lugha ya Pili

Makokha, R.M.[1], Ngowa, N. J.[2], Chimerah, R. M.[3], Wallace. S. M.[4]

IKISIRI

Wazungumzi wa lugha ya Kiswahili ambao lugha yao ya kwanza ni Kitachoni hufanya makosa katika maandishi na matamshi yao kwa lugha ya Kiswahili. Makala haya yamefafanua makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wanaozungumza Kitachoni wanapojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Wanafunzi lengwa walikuwa wa kiwango cha gredi ya 7 na 8 walio ndani ya mtaala unaojikita katika misingi ya Umilisi na Utendaji (Competency Based Education (CBE). Lengo mahsusi la kuyafafanua makosa yaliyofanywa na wanafunzi hawa ni kuweka wazi michakato mahsusi ya kimofofonolojia inayo - dhihirika na kupendekeza njia za kutatua kitaaluma. Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi makosa iliyoasisiwa na Corder (1967) kama mwongozo wa kuchambua makosa yaliyofanywa na wanafunzi wateule katika gredi ya 7 na 8 na kisha kupendekeza njia mwafaka za kuwaepusha wasomaji hawa kuyafanya makosa ya kimofofonolojia katika kazi zao za kimaandishi na pia za kimazungumzo. Kutokana na udurusu wetu maktabani tulibaini kuwa kuna pengo la kiisimu katika ulinganishi wa lugha ya Kitachoni ambayo ni lugha ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili na jambo hili ndilo lililotupelekea kutafitia mada hii ili kuliziba pengo hili la kitaaluma.

Istilahi Maalum: Lugha ya kwanza, Lugha ya pili, Uchanganuzi Makosa, Mofofonolojia, Mtalaa wa Umilisi na Utendaji.

1.0 Utangulizi

Kuanzia miaka ya 1993 hadi 2015, watafiti wengi wamechunguza makosa wakijikita kwenye lugha za kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Haja ya kuitafiti lugha ya Kiswahili inatokana na ukweli kuwa ni muhali kupuuza umuhimu wa lugha hii sio tu nchini Kenya bali pia katika jamii ya kimataifa. Lugha ya Kiswahili imekua, ikaenea na ikapanua mawanda yake ya kimatumizi tangu ipangwe na kusanifishwa. Lengo la watafiti waliochunguza lugha hizi kwanza na namna zinaiathiri lugha ya Kiswahili ni kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inaandikwa na kutamkwa kwa njia ambazo zinastahili. Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu ulifanywa kuhusu namna wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kitachoni wanahawilisha makosa ya kimofofonolojia kutoka lugha ya Kitachoni hadi kwa lugha ya Kiswahili na kusababisha athari hasi kwa kukua kwa lugha ya Kiswahili.

1.2 Fonimu za Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ina fonimu aina mbili; yaani irabu na konsonanti. Katika makala haya tumeonyesha sifa za irabu na konsonanti za Kiswahili na namna sauti hizi zinavyotumika katika maneno mbalimbali ya lugha ya Kiswahili na wanafunzi wa gredi ya 7 na 8, hali ambayo inasababisha kutokea kwa makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa kazi za wanafunzi hawa.

1.2.1 Irabu za Kiswahili

Sauti ya vokali au irabu inatamkwa bila kuzuilia hewa katika ala mbalimbali za kutamkia sauti. Vigezo mbalimbali vya fonolojia vinavyotumiwa katika uainishaji wa vokali ni; mwinuko wa ulimi, sehemu ya ulimi na hali ya midomo. Sehemu ya ulimi huwa inaonyesha mahali pa ulimi ambapo panahusika wakati irabu ama vokali zinapotamkwa. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ya Hooper (1976) inaeleza kuwa sauti zina sifa ambazo huwekwa katika mpangilio ambao unaitwa matriki. Kila kundi la sifa huwa linaelezea maana ya irabu au konsonanti fulani. Sifa hizi huwa zinawakilishwa na ishara ya [+] ili kuonyesha ya kuwa sifa hiyo ipo au ishara ya [-] kuonyesha ya kuwa hiyo sifa haipo. Matumizi ya hii nadharia iliyo ya fonolojia zalishi kwa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa yalikuwa na manufaa mengi sana kwa utafiti huu. Yalionyesha matumizi ambayo si sahihi yaliyotokea kwa konsonanti na irabu katika maneno mbalimbali.

Sifa za irabu hizi ni kama zifuatazo:

/a/	/ɛ/	/ɔ/
+ irabu	+ irabu	+ irabu
-nyuma	- chini	- chini
+ chini	- juu	- juu
-mviringo	-mviringo	+ mviringo
-mbele	- nyuma	+ nyuma

/i/	/u/
+ juu	+ juu
+ irabu	+ irabu
-mviringo	+ mviringo
-nyuma	+ nyuma

1.2.2 Konsonanti za Kiswahili

Habwe na Karanja (2004:28) wanaeleza sauti ya konsonanti kuwa ni sauti ambayo inatamkwa wakati ambapo hewa inayotoka kwenye mapafu inazuiliwa ama kabisa au kidogo na kuifanya nafasi ambayo hewa hupitia kuwa ndogo na kuifanya hewa kupita kwa njia ya mkwaruzo.

Sifa bainifu za konsonanti za Kiswahili kama alivyoeleza Richard S. Mgullu (1999) ni:

1. Ukonsonanti
2. Namna ya kuitamka
3. Mahali pa kuitamkia
4. Mtikisiko wa nyuzi za sauti
5. Unazali

Lugha ya Kiswahili ina aina zifuatazo za konsonanti:

a.Vipasuo

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa vipasuo ni sauti ambazo hutamkwa wakati hewa inajaa au inafungiwa katika ala ya kutamkia ambayo huizuia na kusababisha mpasuko inapoachiliwa au inapotolewa nje. Lugha ya Kiswahili ina vipasuo /b/, /p/, /g/, /k/, /d/, /t/, na /ɟ/.

Sifa za vipasuo ni kama zifuatazo:

/p/	/b/	t/
+ konsonanti	+ konsonanti	+ konsonanti
+ kizuiwa	+ kizuiwa	+ kizuiwa
+ midomoni	+ midomoni	+ midomoni
- unazali	- unazali	- unazali
- ghuna	+ ghuna	- ghuna

/d/	/ɟ/	/k/
+ konsonanti	+ konsonanti	+ konsonanti
+ kizuiwa	+ kizuiwa	+ kizuiwa
+ ufizi	+ Kaa kaa gumu	+ Kaa kaa laini
- unazali	- unazali	- unazali
+ ghuna	+ ghuna	- ghuna

/g/
+ konsonanti
+ kizuiwa
+ Kaa kaa laini
- unazali
+ ghuna

b. Vikwamizwa/Vikwaruzo

Sauti ya vikwamizo au vikwaruzo huwa inatamkwa wakati hewa inapokuwa imezuiliwa kwenye ala za kutamkia sauti kwa kiasi tu na si kufungiwa kabisa. Vikwamizo vya lugha ya Kiswahili ni /f/, /v/, /s/, /z/, /θ/, / /, /h/, /ð/ na /ð/. Vikwamizo au vikwaruzo vya lugha ya Kiswahili vina sifa zifuatazo;

/f/	/v/	/s/
+ konsonanti	+ konsonanti	+ konsonanti
+ kikwamizwa	+ kikwamizwa	+ kikwamizwa
+ midomo na meno	+ midomo na meno	+ ufizi
- unazali	- unazali	- unazali
- ghuna	+ ghuna	- ghuna

/z/	/ʃ/	/h/
+ konsonanti	+ konsonanti	+ konsonanti
+ kikwamizwa	+ kikwamizwa	+ kikwamizwa
+ ufizi	+ Kaa kaa laini	+ glota
- unazali	- unazali	- nazali
+ ghuna	- ghuna	- ghuna

/ð/	/θ/	/ɣ/
+ konsonanti	+ konsonanti	+ konsonanti
+ kikwamizwa	+ kikwamizwa	+ kikwamizwa
+ meno	+ meno	+ Kaa kaa laini
- unazali	- unazali	- unazali
+ ghuna	- ghuna	+ ghuna

c. Kipasuo kwamizo / Kipasuo kwaruzo

Habwe na Karanja (2004:34) wanasema kuwa sauti ya kipasuo kwaruzo hutamkwa wakati hewa inafungiwa kabisa katika sehemu ya kutamkia kisha inaachiliwa kwa ghafla.

Sauti hii ni /tʃ/

Sifa za hiki Kipasuo- kwamizo /tʃ/ni:

/tʃ/

+ konsonanti
+ kizuia kwamizwa
+ Kaa kaa gumu
- unazali
- ghuna

d. Nazali

Sauti ya nazali huwa inatamkwa wakati hewa inapitia kwenye kinywa na pua. Lugha ya Kiswahili ina nazali nne ambazo ni /m/, /n/, /ɲ/ na /ŋ/.
Sifa za nazali ni:

/m/	/n/
+ konsonanti	+ konsonanti
+ nazali	+ nazali
+ midomo	+ ufizi
+ unazali	+ unazali
+ ghuna	+ ghuna

/ɲ/	/ŋ/
+ konsonanti	+ konsonanti
+ nazali	+ nazali
+ Kaa kaa gumu	+ Kaa kaa laini
+ nazali	+ unazali
+ ghuna	+ ghuna

e. Likwidi

Likwidi zinapotamkwa hewa huwa inazuiliwa kiasi tu kisha inaachiliwa ipite kando kando ya ulimi. Lugha ya Kiswahili ina likwidi za aina mbili ambazo ni kimadende /r/ na kitambaza /l/.

Likwidi zina sifa zifuatazo:

/r/	/l/
+ konsonanti	+ konsonanti
+ kimadende	+ kitambaza
+ ufizi	+ ufizi
- unazali	- unazali
+ ghuna	+ ghuna

f. Viyeyusho/Nusu- irabu

Sauti ya nusu - irabu wakati inatamkwa huwa hewa inaruhusiwa kupita sehemu ya kinywa bila kuzuiliwa na ala zozote za sauti. Sauti ya nusu- irabu katika lugha ya Kiswahili huwa ni mbili ambazo ni; /j/ na /w/. Sauti /w/ hutamkiwa midomoni nayo sauti /j/ hutamkiwa kwenye kaakaa gumu. Sauti hizi zina sifa zifuatazo;

/w/	/j/
+ konsonanti	+ konsonanti
+ nusu irabu	+ nusu irabu
+ midomoni	+ midomoni
-unazali	-unazali
+ ghuna	+ ghuna

1.3 Fonimu za Kitachoni

Lugha ya Kitachoni pia ina fonimu za irabu na konsonanti. Makala haya yameonyesha sifa za irabu na konsonanti za lugha lugha ya Kitachoni.

1.3.1 Konsonanti za lugha ya Kitachoni

Lugha ya Kitachoni ina konsonanti kumi na saba ambazo ni:

/t/, /s/, /p/, /f/, /v/, /l/, /x/, /k/, /tʃ/, /j/, /r/, /m/, /ŋ/, /ɲ/, /n/, /w/, /ʃ/

Konsonanti za lugha ya Kitachoni zina sifa bainifu zifuatazo:

a.Vipasuo/Vizuiwa

Lugha ya Kitachoni ina vipasuo ama vizuiwa vitatu ambavyo ni: /p/, /t/ na /k/. Sifa za vizuiwa hivi ni:

/p/	/t/	/k/
+ konsonanti	+ konsonanti	+ konsonanti
+ Kizuiwa	+ Kizuiwa	+ Kizuiwa
+ Midomoni	+ Midomoni	+ Kaakaa laini
- Unazali	- Unazali	- Unazali
- Ghuna	- Ghuna	- Ghuna

b. Vikwaruzo/Vikwamizo

Wakati wa kuzitamka sauti hizi, huwa ala zinazotumika katika kutamka zinakaribiana kisha hewa huwa inaachiliwa na kutoka polepole kwa hali ambayo ni ya kukwamiza.

Mifano ya vikwaruzo vya Kitachoni ni /f/, /v/, /x/, /s/, na /ʃ/

Vikwaruzo vya lugha ya Kitachoni vina sifa zifuatazo ambazo zimeorodheshwa hapa chini

/v/

[+ konsonanti
+ Kikwamizwa
+ Midomo na Meno
+ Ghuna
- Unazali]

/f/

[+ konsonanti
+ Kikwamizwa
+ Midomo na Meno
- Ghuna
- Unazali]

/s/

[+ konsonanti
+ Kikwamizwa
+ Ufizi
- Ghuna]

/x/

[+ konsonanti
+ Kikwamizwa
+ Kaakaalaini
- Unazali
- Ghuna]

/ʃ/

[+ konsonanti
+ Kikwamizwa
+ Kaakaa na ufizi
- Unazali
- Ghuna]

c. Kipasuo - Kwamizo

Sauti hii pia huitwa kipasuo kwaruzo. Wakati wa kuitamka, hewa huwa inakwamizwa kisha baadaye huachiliwa na kutoka katika hali ambayo inasababisha kutokea kwa mpasuko.

Kitachoni ni lugha ambayo ina kipasuo-kwamizo kimoja na ambacho ni /tʃ/. Kipasuo-kwamizo hiki huwa kinatamkiwa kwenye sehemu ya kaakaa gumu na sauti hii si sauti ghuna. Sifa za kipasuo kwamizo hiki ni:

Sauti hii pia huitwa kipasuo kwaruzo. Wakati wa kuitamka, hewa huwa inakwamizwa kisha baadaye huachiliwa na kutoka katika hali ambayo inasababisha kutokea kwa mpasuko.

Kitachoni ni lugha ambayo ina kipasuo-kwamizo kimoja na ambacho ni /tʃ/. Kipasuo-kwamizo hiki huwa kinatamkiwa kwenye sehemu ya kaakaa gumu na sauti hii si sauti ghuna. Sifa za kipasuo kwamizo hiki ni:

/tʃ/

[+ konsonanti
+ Kipasuo kwamizo
- Unazali
+ Kaakaa gumu
+- Ghuna]

d. Nazali/Ving'ong'o

Wakati wa kuzitamka sauti za nazali, hewa huwa inazuiliwa na baadaye inaachiliwa kupitia kwenye pua. Lugha ya Kitachoni ina nazali aina nne ambazo ni /n/, /m/, /ŋ/ na /ɲ/ Sifa za nazali za Kitachoni ni kama zifuatazo:

/m/

[+ konsonanti
+ Nazali
+ Midomoni
+ Ghuna
+ Unazali]

/n/

[+ konsonanti
+ Nazali
+ Ufizi
+ Ghuna
+ Unazali]

/ɲ/

[+ konsonanti
+ Nazali
+ Kaa kaa Gumu
+ Ghuna
+ Unazali]

/ŋ/

[+ konsonanti
+ Nazali
+ Kaa kaa laini
+ Ghuna
+ Unazali]

e. Likwidi

Lugha ya Kitachoni ina likwidi za aina mbili ambazo ni kitambaza /l/ na kimadende /r/ Katika kuitamka sauti ya /l/ ncha ya ulimi huwa inaguza sehemu ya ufizi halafu hewa inapitia

Kwa sehemu ya pembeni mwa ulimi na kwa upande mwingine, wakati wa kuitamka /r/ ncha ya ulimi huwa inapigapiga ufizi. Sifa za likwidi za lugha ya Kitachoni ni kama zifuatazo,

/l/

[+ konsonanti
+ Kitambaza
+ Ufizi
+ Ghuna
-Unazali]

/r/

[+ konsonanti
+ Kimadende
+ Ufizi
+ Ghuna
- Unazali]

f. Nusu irabu/Viyeyusho

Hizi ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka ala za kutamkia hukaribiana kisha hewa hupitishwa kati ya ala hizo bila kuzuiliwa. Lugha ya Kiswahili ilibainika kuwa na sauti za nusu irabu mbili ambazo ni /w/ na /j/

Sifa za Nusu irabu za Kitachoni ni:

/w/
[+ Nusu Irabu
+ Midomoni
+ Konsonanti
+ ghuna
- unazali]

/j/
[+ konsonanti
+ Nusu irabu
+ Kaakaa Gumu
+ Ghuna
- Unazali]

Konsonanti za Kitachoni zimewakilishwa kiothografia na kifonetiki kama zinavyoonyeshwa katika maneno ya Kitachoni hapa chini.

Uwakilishi kiothografia	Mnukuu	Neno la Kitachoni	Tafsiri
V	/v/	/ a**v**ɛ:xɔ /	Ukoo
P	/p/	/ **p**apa /	Baba
F	/f/	/ ɔlu**f**u /	Kifo
T	/t/	/ li**t**u:ka /	Duka
S	/s/	/ ɛ**s**iɛɣɔ /	Ufagio
Ch	/tʃ/	/ ɛ**tʃ**ai /	Chai
Kh	/x/	/ li**x**ɔva /	Ngozi
K	/k/	/ ɔmu**k**unda /	Shamba
L	/l/	/ li**l**ɔva /	Mchanga
R	/r/	/ ɔmu**r**wɛ /	Kichwa
W	/w/	/ ɔ**l**wana /	Utoto
Y	/j/	/ livu**j**u /	Yai
M	/m/	/ **m**a**j**i /	Mama
N	/n/	/ ɛli**n**ɔ /	Jino
SH	/ʃ/	/ e**ʃ**uka /	Shuka
NG'	/ŋ/	/ li**ŋ**a:ŋa /	Ndege
Ny	/ɲ/	/ i**ɲ**aɲa /	Nyanya

1.3.2 Irabu za Kitachoni

Lugha ya Kitachoni ina irabu 10 ambapo, irabu 5 ni fupi na irabu 5 ni ndefu. Irabu /a/, /e/, /i/, /ɔ/, /u/ ni Irabu fupi na /a:/, /e:/, /i:/, /ɔ:/, /u:/ ni irabu ndefu.

Irabu za Kitachoni zina sifa zifuatazo

/a/
[+ irabu
- nyuma
- ndefu
- mviringo
- juu]

/ɛ/
[+ irabu
- nyuma
- ndefu
- mviringo
- juu]

/i/
[+ irabu
- nyuma
- ndefu
- mviringo
+ juu]

/a:/
[+ irabu
- nyuma
+ ndefu
-mviringo
- juu]

/ɛ:/
[+ irabu
- nyuma
+ ndefu
- mviringo
- juu]

/i:/
[+ irabu
- nyuma
+ ndefu
- mviringo
+ juu]

/ɔ/
[+ irabu
+ nyuma
-ndefu
-juu
+ mviringo]

/u/
[+ irabu
+ nyuma
- ndefu
+ juu
+ mviringo]

/ɔ:/
[+ irabu
+ ndefu
+ nyuma
+ mviringo
-juu]

/u:/
[+ irabu
+ ndefu
+ nyuma
+ mviringo
+juu]

1.4 MAKOSA YA KIMOFOFONOLOJIA KATIKA KAZI ZA WANAFUNZI

Tumechunguza makosa tofauti tofauti ambayo wanafunzi walio Watachoni wameyafanya katika kazi andishi na tamkwa katika shule za upili tatu ambazo ni shule ya upili ya Maturu, shule ya upili ya Lwandeti D.E.B na shule ya upili ya Lukhokho. Hizi ni shule ambazo hupatikana katika Wadi ya Lwandeti kutoka kaunti ya Kakamega.

Makosa ambayo yalifanywa na watafitiwa ambayo yalisababisha kutokea kwa makosa ya kimofofonolojia ni kama ifuatavyo:

1.4.1 Uchopekaji

Iribemwangi (2010) anaelezea kuwa kuchopeka ni kuongeza sauti za irabu ama sauti za konsonanti ambazo hazistahili kuwa katika neno unde ila mtumiaji huwa anaziongeza

kwa sababu ya kuwa labda katika lugha yake sauti hii ipo ama kutokana na mazoea ya kuitumia.

Lugha ya Kiswahili inazo silabi funge kutokana na kukopa kwa baadhi ya maneno kutoka kwa lugha zingine kama Kiingereza, Kiarabu na kadhalika ila katika lugha ya Kitachoni silabi funge haipo na ndiposa wanafunzi wengi walilazimisha kuipachika irabu ili kuafikia muundo wa lugha yao waliyoizoea. Mifano ya kijumla ya upachikaji wa irabu ama konsonanti katika aina za maneno mbalimbali ni kama vile:

a. Uchopekaji wa sauti /h/

Konsonanti /h/ ni sauti ya Kiswahili ambayo inatamkiwa katika sehemu ya koromeo. Licha ya kuwa konsonanti hii haipo katika lugha ya Kitachoni wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walitatizika kutambua matumizi yake na hivyo kuipachika sehemu isiyofaa katika baadhi ya maneno ambayo waliyatumia katika insha zao ifuatavyo:

Kiswahili	**Uchopekaji**	**Aina ya neno**
Ofisi	/ **h**ofisi /	Nomino
Asubuhi	/ **h**asubuhi /	Nomino
Asante	/**h**asante/	Nomino
Ona	/**h**ona/	Kitenzi
Omba	/**h**omba/	Kitenzi
Ota	/**h**ota /	Kitenzi
Ua	**/hua/**	Kitenzi
Uza	**/huza/**	Kitenzi

Makosa ya uchopekaji ya aina hii ya kuchopeka konsonati /h/ katika maneno ya Kiswahili yalidhihirika zaidi katika vitenzi na nomino za Kiswahili vinavyoanza kwa irabu kwa mfano *himba* badala ya *imba*

b. Uchopekaji wa kiyeyusho /w/

Sauti ya nusu irabu ama kiyeyusho ya /w/ pia ilichopekwa katika baadhi ya maneno ambayo yaliandikwa na kutamkwa na watafitiwa wa lugha ya Kitachoni jambo ambalo lilisababisha kutokea kwa makosa ambayo ni ya kimofofonolojia katika kazi za watafitiwa hawa. Licha ya kuwa lugha ya Kitachoni ina sauti hii ya /w/ katika konsonanti za lugha hizi watafitiwa walikanganywa na matumizi ya sauti hii na hivyo kuitumia sauti hii ya nusu irabu visivyo ifuatavyo:

Kiswahili	**Uchopekaji**	**Aina ya neno**
Chukua	/ chuku**w**a /	Kitenzi
Pakua	/ paku**w**a /	Kitenzi
Toa	/to**w**a /	Kitenzi
Fua	/fu**w**a/	Kitenzi
Tua	/tu**w**a/	Kitenzi

Wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walichopeka sauti /w/ katikati ya irabu mbili katika maneno ili kuvunja muundo huu na kuhifadhi muundo wa konsonanti-irabu kwa mfano neno *toa* waliandika *towa.*

c. Uchopekaji wa kiyeyusho /j/

Kutokana na data ambayo tulipata kutoka kwa wanafunzi walio wa gredi ya 7 na 8 kutoka katika shule za sekondari msingi ya Mutenyo, Lukhokho na Maturu ilibainika kuwa wanafunzi wenye asili ya Kitachoni waliweza kupachika sauti ya nusu irabu ya /j/ katika baadhi ya maneno jambo ambalo lilisababisha kutokea kwa makosa yaliyo ya kimofofonolojia miongoni mwao. Kwa mfano:

Kiswahili	**Uchopekaji**	**Aina ya neno**
Kilio	/ kili**j**o /	Nomino
Zuia	/ zui**j**a /	Kitenzi
Kisia	/kisi**j**a/	Kitenzi
Julia	/tʃuli**j**a/	Kitenzi
Sikia	/siki**j**a/	Kitenzi
Tulia	/tuli**j**a/	Kitenzi

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walichopeka konsonanti ya kiyeyusho ya /j/ kabla ya irabu ili kuunda muundo wa silabi pendwa ya (KI) katika neno hili jambo ambalo lilisababisha kutokea kwa makosa ya kimofofonolojia.

1.4.2 Ubadala wa Sauti

Kitachoni na lugha ya Kiswahili zinazo sauti za irabu na Konsonanti ambazo kwa njia moja ama nyingine kuna zile ambazo zinafanana na zile ambazo ni zinatofautiana. Tumeonyesha njia mbalimbali ambazo watafitiwa wetu wa lugha ya Kitachoni waliathirika katika ujifundishaji wa Kiswahili sanifu kwa kutumia sauti mbadala katika maneno ambayo waliandika hivyo kusababisha makosa ya kimofofonolojia kwa mfano katika aina mbalimbali za maneno mifano ya jumla iliyojitokeza ni ifuatavyo:

Aina ya neno	Kiswahili	Ubadala wa sauti	Sauti Mbadala
Nomino	Baba	**p**a**p**a	/p/
Kitenzi	anakuja	anaku**ch**a	/ch/
Kivumishi	mahali hapa	mahali ha**b**a	/b/
Kiwakilishi	sisi	**z**i**z**i	/z/
Kihusishi	ndani ya	n**t**ani ya	/t/
Kiunganishi	ijapokuwa	i**ch**apokua	/ch/
Kielezi	temebea pole pole	tembea **b**ole **b**ole	/b/

Kutokana na mifano tuliyoonyesha hapa juu, wengi wa wanafunzi walikuwa wakibadilisha sauti isiyofaa na kutumia sauti ambayo inapatikana katika lugha ya Kitachoni. Hapa sauti ya lugha ya Kitachoni ilihamishwa na kuingizwa katika lugha ya Kiswahili mahali ambapo haifai na jambo hili lilisababisha makosa ya kimofofonolojia. Makosa ya kubadilisha sauti yalipatikana kwa wingi katika insha za watafitiwa. Hapa chini tumeonyesha mifano ya sauti zilizobadilishwa na wanafunzi hawa wakiwa katika mchakato wa kujifundisha lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo:

a. Ubadala wa Konsonanti

Lugha ya Kiswahili na ile ya Kitachoni zina konsonanti ambazo zinafanana na konsonanti ambazo zinatofautiana. Na ni kutokana na hali hii ambapo wanafunzi wa Kitachoni walio katika gredi ya 7 na 8 waliweza kubadilisha baadhi ya konsonanti na kutumia konsonanti zinazopatikana katika lugha yao ya kwanza ya Kitachoni. Hii ni hali ya kuathirika na lugha yao ya kwanza hivyo basi kuhamisha konsonanti hizo kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, wanafunzi hawa walibadilisha konsonanti zifuatazo katika data ambayo ilipatikana katika insha za wanafunzi:

1. Matumizi ya fonimu /tʃ/ badala ya /ɟ /

Lugha ya Kitachoni na lugha ya Kiswahili zinatofautiana zaidi hasa katika matumizi ya sauti ya /tʃ/ na sauti ya /ɟ/. Ikumbukwe kwamba lugha ya Kiswahili ina sauti /tʃ/ na sauti ya /ɟ/. lakini lugha ya Kitachoni haina sauti /ɟ/. bali ina sauti /tʃ/ pekee. Kwa hivyo, katika maneno ambayo yalistahili kuwa na sauti /ɟ/ wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walio katika gredi ya 7 na 8 waliibadilisha sauti hii na kutumia sauti /tʃ/ iliyo katika lugha yao ili kurahisisha matamshi yao. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya makosa yaliyodhihirika.

Kiswahili	Ubadala wa sauti	Aina ya neno
/ **ɟ**umapili /	/**tʃ**umapili/	Nomino
/ **ɟ**embɛ /	/**tʃ**ɛmbɛ/	Nomino
/ **ɟ**ambazi /	/**tʃ**ambazi/	Nomino
/ **ɟ**ɛla /	/**tʃ**ɛla/	Nomino

/ ɟɛuri /	/tʃɛuri/	Nomino
/ ɟaza /	/tʃasa/	Nomino
/ ɟumatatu /	/tʃumatatu/	Nomino
/ ɟambazi /	/tʃambazi/	Nomino
/ ɟɛshi /	/tʃɛshi/	Nomino
/ ɟasusi /	/tʃasusi/	Nomino
/ ɟamuhuri /	/tʃamuhuri/	Nomino
/ ɟua /	/tʃua/	Kitenzi
/ wafugaɟi /	/wafugatʃi/	Nomino

Wanafunzi wenye asili ya Kitachoni waliunda sauti hii mbadala hivyo kuleta muundo mpya ufuatao:

Kanuni : /ɟ/ → /tʃ/ + i

2. Matumizi ya /p/ badala ya /b/

Corder (1981) alieleza kwamba utendaji wa makosa katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili unapaswa kuangaliwa kwa mtazamo chanya kwa kuwa ndio humwezesha anayejifunza lugha yoyote kufikia umilisi wa lugha lengwa. Maelezo haya ni faafu sana katika utafiti huu kwa kuwa faafu sana katika utafiti huu kwa kuwa matumizi ya sauti hizi za vipasuo. Kama tulivyotaja hapo awali, lugha ya Kitachoni inayo sauti /p/ bali haina sauti /b/ katika konsonanti zake. Na kwa upande mwingine lugha ya Kiswaili inazo konsonanti hizi mbili. Katika matumizi yake, wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walio katika gredi ya 7 na 8 walionyesha kubadilisha kwa sauti /b/ na kutumia sauti /p/ katika mifano ya maneno yao ifuatavyo:

Kiswahili	Ubadala wa sauti	Aina ya neno
Baba	**P**apa	Nomino
Baadaye	**P**aadaye	Kielezi
Barafu	**P**arafu	Nomino
Bunduki	**P**unduki	Nomino
Bao	**P**ao	Nomino
Bafuni	**P**afuni	Kielezi
Breki	**P**ureki	Nomino
Babu	**p**apu	Nomino
	Paraka	Nomino
mkabala na	Mkapala na	Kihusishi

Kanuni : /b/ → /p/ / + i

Sauti za /b/ na /p/ zina ukuruba mkubwa sana kifonetiki na ndiposa katika matumizi yake wanafunzi waliweza kutatizika kuzitofautisha ila ni wazi kwamba sauti /p/ ni sighuna ilhali sauti /b/ ni sauti ghuna. Hivyo, wanafunzi wengi walishindwa kutofautisha sauti hizi kimatamshi na kimaandishi jambo ambalo lilisababisha wao kuyafanya makosa yaliyo ya kimofofonolojia kutokea.

3.Matumizi ya /b/ badala ya /p/

Hata hivyo, licha ya kuwa wanafunzi wengi waliathirika kwa kubadilisha sauti /b/ na kuitumia kama /p/ kunao wanafunzi ambao walibadilisha sauti /p/ na kuitumia kama /b/ ifuatavyo;

Kiswahili	Ubadala wa sauti	Aina ya neno
Pesa	**B**esa	Nomino
Pima	**B**ima	Kitenzi
Pita	**B**ita	Kitenzi
Posa	**B**osa	Nomino
Pika	**B**ika	Kitenzi
Pongezi	**B**ongezi	Nomino
Pata	**B**ata	Nomino

Watafitiwa walikanganywa na matumizi ya sauti hizi mbili za vipasuo na hivyo kusababisha makosa haya ya kimofofonolojia kutokea kama tulivyoonyesha hapo juu. Hii ni kutokana na ukaribu wa matamshi wa sauti hizi mbili hivyo kusababisha wanafunzi kutamka ile iliyo rahisi kwao.

Kanuni : /p/ → /b/ / + i

4.Matumizi ya /d/ badala ya /t/

Kutokana na data ya watafitiwa wetu, ilibainika kwamba wengi wa wanafunzi waliweza kubadilisha matumizi ya sauti ya kipasuo /t/ na katika nafasi yake wanafunzi hawa walitumia sauti /d/ mchakato wa ubadilishaji huu ulisababisha wengi wa wanafunzi kuyafanya makosa ambayo ni

ya kimofofonolojia kutokea katika kazi andishi na kazi za kimatamshi ambazo tulikusanya kutoka kwao. Kwa mfano:

Kiswahili	Ubadala wa sauti	Aina ya neno
/ tɔa /	/dɔa/	Kitenzi
/ tɛmbɛa /	/ dɛmbɛa /	Kitenzi
/ taka /	/daka/	Nomino
/ timu /	/dimu/	Nomino

Kutokana na data ya watafitiwa, ni wazi kwamba wanafunzi hawa walibadilisha sauti hizi na hivyo kusababisha kutokea kwa makosa haya ya Kimofofonolojia kuwepo. Mabadiliko katika sauti hizi ziliundwa ifuatavyo:

Kanuni : /t/ ⟶ /d/ / + i

5.Matumizi ya sauti /k/ badala ya /g/

Data iliyopatikana kutoka kwa watafitiwa ilibainisha kuwa, wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walibadilisha matumizi ya sauti /g / na badala yake wakaitumia sauti /k/. Lugha ya Kitachoni ina sauti sighuna /k/ ila haina sauti ghuna /g/. Ni kutokana na hali hii ambapo wanafunzi walibadilisha matumizi ya sauti hii na hivyo kusababisha kutokea kwa makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa kazi andishi na za kimatamshi ifuatavyo:

Kiswahili	Ubadala wa Sauti	Aina ya neno
/ Gazɛti /	/ kasɛti /	Nomino
/ Gari /	/ kari /	Nomino
/ Mzigɔ /	/ msikɔ /	Nomino
/ Ndɛgɛ /	/ ndɛkɛ /	Nomino
/ Gundua /	/ kundua /	Kitenzi
/ Mhɔgɔ /	/ muhɔkɔ /	Nomino
/ Gazɛti /	/ kasɛti /	Nomino
/ Gundua /	/ kundua /	Kitenzi
/ Gari /	/kari/	Nomino
/ Mzigɔ /	/ mzikɔ /	Nomino
/ Mtɛgɔ /	/ mtɛkɔ /	Nomino
/ Ganda /	/ kanda /	Nomino
/ Ndɛgɛ /	/ ndɛkɛ /	Nomino

Data ya watafitiwa wetu ilionyesha kuwa wana funzi wenye asili ya Kitachoni hutumia sauti /k/ kwa kuwa ina urahisi wa kuitamka ikilinganishwa na sauti /g/ na hivyo mabadiliko haya yalisababisha kuundwa kwa muundo ufuatao wa silabi:

Kanuni : /g/ ⟶ /k/ / + i

Makosa ya aina hii yalikuwa mengi miongoni mwa wazungumzaji wa Kitachoni wanapojifundisha lugha ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili.

1. **Matumizi ya sauti /k/ badala ya /ɣ/**

Wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walitumia sauti /k/ katika sehemu ambapo palihitajika kutumia sauti /gh/ katika insha na maandishi yao jambo ambalo lilisababisha kutokea kwa makosa ambayo ni ya kimofofonolojia kutokea.

Mifano ifuatayo ilitumika na watafitiwa wetu.

Neno sahihi la Kiswahili	Ubadala wa sauti	Aina ya neno
/ ɣɔrɔfa /	/ korɔfa /	Nomino
/ ɣarama /	/ karama /	Nomino
/ luɣa /	/ luka /	Nomino
/ ɣali /	/ kali /	Kivumishi
/ ɣaðabu /	/ katθapu /	Nomino
/ ʃaɣalabaɣala /	/ ʃakalapakala /	Kielezi
/ ɣairi /	/ kairi /	Kielezi

Sauti /ɣ/ na sauti /k/ hutamkiwa katika sehemu ya kaakaa laini na pia hizi ni sauti za vikwaruzo katika lugha ya Kiswahili. Sauti /k/ inapatikana katika konsonanti za Kitachoni ilhali sauti /ɣ/ haipo katika konsonanti za lugha ya Kitachoni na jambo hili liliwafanya wanafunzi wanaojifundisha lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili kufanya makosa kwa kubadilisha matumizi ya sauti hizi kama tulivyoonyesha katika mfumo wa muundo wa silabi ifuatavyo:

Kanuni : /ɣ/ ⟶ /k/ / + i

7. Matumizi ya sauti /s/ badala ya /z/

Wanafunzi wenye asili ya Kitachoni katika mchakato wa kujifundisha Kiswahili kama lugha yao ya pili waliweza kutumia sauti /s/ mahali ambapo palihitajika kutumika kwa sauti /z/ kutokana na data ambayo tulipata kutoka kwa mandishi na matamshi ya watafitiwa hawa.

Ikumbukwe kwamba sauti hizi zina ukuruba wa karibu kabisa kifonetiki kwa kuwa ni vikwaruzo ambazo zinatamkiwa sehemu ya ufizi. Hivyo, ziliwatatiza wanafunzi katika matumizi yake na kusababisha makosa ya kimofofonolojia kutokea ifuatavyo:

Neno sahihi	Ubadala wa sauti	Aina ya neno
/ **z**aburi /	/ **s**apuri /	Nomino
/ manda**z**i /	/ manda**s**i /	Nomino
/ **z**ima /	/ **s**ima /	Kitenzi
/ **z**ɔɛ**z**i /	/ **s**ɔɛ**s**i /	Nomino
/ **z**ɛmbɛa /	/ **s**ɛmbɛa /	Kitenzi
/ ha**z**ipɔ /	/ ha**s**ipɔ /	Kitenzi
/ pum**z**i /	/ pum**s**i /	Nomino
/ m**z**uri /	/ mu**s**uri /	Kivumishi

Ni bayana kuwa wanafunzi wenye asili ya Kitachoni wanaojifundisha lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili waliweza kuathirika zaidi katika matumizi sauti hii ya /s/ palipohitajika wao kutumia sauti /z/ sababu ikiwa kwamba lugha ya Kitachoni ina sauti /s/ ila haina sauti /z/ katika konsonanti zake. Kanuni ifuatayo ya silabi ilitumika katika mabadiiko haya:

Kanuni : **/z/** ⟶ /s/ / + i

Mchakato huu wa ujifundishaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili uliwalazimu baadhi ya wanafunzi kuhamisha vipengele fulani vya lugha ya Kitachoni hadi kwa lugha ya Kiswahili, kunao wanafunzi ambao walipachika sauti ama herufi katika maneno ya Kiswahili kwa nia isiyofaa, pia, kunao wanafunzi ambao walibadilisha umbo la neno kwa kutumia sauti mbadala.

1.43 Kupendekeza Mikakati ya Kuyarekebisha Makosa

Makosa yaliyopatikana katika utafiti huu yana athari kubwa kwa wanafunzi. Athari zifuatazo zimeweza kuelezwa wazi na na njia za kurekebisha makosa haya kupendekezwa.

1.4.4 Athari za Makosa ya Kimofofonolojia

i) Athari ya kuanguka mtihani

Wanafunzi wanaojipata wanafanya makosa ya kimofofonolojia ya lugha huwa wanakosolewa katika mitihani wa kitaifa na kwa hali hii inawafanya kuanguka mitihani hii. Makosa ya kimofofonolojia yanaweza kubadilisha maana ya maneno hivyo basi kupotosha ujumbe, hasa katika uandishi wa insha, karatasi la sarufi na matumizi ya lugha na hata karatasi la fasihi la mtihani wa kitaifa. Vilevile, makosa haya yanapopatikana katika sehemu ya lugha, yaa sarufi, hukosolewa kwa kuonyesha kwamba mwanafunzi amekosea herufi za maneno kwa hivyo hajamudu lugha. Wanafunzi wanapopata alama za chini za lugha hushukishwa alama zingine zote za mitihani yote na hali hii huwafanya wakose kozi ambazo wangependa kufanya katika usomi wao. Kwa hivyo, hii ni athari hasi kwa wanafunzi hivyo basi inapaswa itafutiwe suluhu.

ii) Athari ya kutoaminika katika Mazungumzo

Mwanafunzi au mtu yoyote yule anapofanya makosa mengi katika lugha hukosa kuaminika kwa yale anayoyazungumza. Aidha hushukiwa kuwa labda hakufanya vizuri katika mitihani kwa hivyo hukosa imani ya kuwa anaweza kufanya jambo lolote. Waajiri wengi humshuku kama kweli anaweza kuajiriwa na kufanya kazi vizuri.

iii) Athari ya aibu ya kutojua lugha

Makosa mengi katika lugha humfanya anayezungumza kuaibika. Hii ni kwa sabau kila mara anapotamka maneno vibaya huchekwa na aidha wanafunzi wenzake na kama ni mwalimu huchekwa na wanafunzi wake. Hali hii humfanya akose ujasiri na kufedheheka.

iv) Athari ya kutokuwa na ujasiri

Kutokana na kuchekwa kwa kila mara, wanafunzi wanaofanya makosa hukosa ujasiri kwa kujieleza na huwa kimya kila wakati kwa kuogopa kuongea na kuchekwa. Hali hii huathiri hata masomo mengine ambayo si ya lugha na hufanya wanafunzi hao hatimaye kuacha shule.

1.4.5 Mapendekezo ya kurekebisha makosa ya kimofofonolojia

Utafiti huu unapendekeza mbinu mbalimbali za kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kama ifutavyo:

i) Kutambua vipengele venye matatizo (makosa) na kurekebisha

Baada ya zoezi lolote linalofanywa la lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili, mwalimu anataki kana atambue vipengele vyenye makosa kwa kila mwanafunzi kwa kuzingatua hatua za nadharia ya Corder (keshatajwa) ili avifanyie marekebisho. Mwalimu anaelekezwa kumshughulik ia kila mwanafunzi kwa kuzingatia upungufu wake wa kipekee. Mwanafunzi wa lugha ya pili anapaswa kuonyeshwa waziwazi vipengele anavyofanya makosa na kurekebishwa.

Mwalimu anahitaji muda mrefu katika somo la lugha ya pili kwa sababu wakati mwingine anahitaji kushughulikia kila mwanafunzi kibinafsi. Mwanafunzi pia anapaswa awekwe katika hali ya uhuru wa kuweza kuzungumza bila kuogopa. Hali hii itamsaidia kuwa na ujasiri wa kuzungumza na kupata uzoefu.

ii) Kufanya mazoezi ya mara kwa mara

Wanafunzi wa lugha ya pili wanaofanya makosa ya kimofofonolojia wanapaswa kufanya mazoezi mengi hasa ya insha. Insha huwa ni zoezi la ubunifu linalomhitaji mwanafunzi kuandika sentensi zake mwenyewe bila kusaidiwa popote. Hali hii inamsaidia mwanafunzi kujikakamua na kuunda sentensi asilia. Huu ni uwanja ambao wanafunzi wengi hufanya makosa kutokana na sentensi asilia wanazoziandika. Kwa hivyo, wanapofanya mazoezi ya kuandika na kusoma ya mara kwa mara, wanajua ni wapi wanapofanya makosa na kujirekebisha kabla ya kuyafanya.

iii)Kuwa na mzungumzi mwenza katika lugha lengwa

Lugha ya pili inahitaji mazungumzo ya mara kwa mara. Inabainika kwamba, wanafunzi waliotafitiwa ni wanafunzi wa shule za kutwa. Hii inamaanisha wanapokuwa shuleni ndio wakati pekee wanapozungumza lugha ya Kiswahili na wakiwa nyumbani wanazungumza lugha ya Kitachoni. Ni wazi kwamba hawana muda wa kutosha wa kuzungumza lugha ya Kiswahili. Mwalimu anaweza kumpatia kila mwanafunzi mzungumzi mwenza ambaye ameimudu lugha ya Kiswahili ili aweze kufanya mazoezi naye. Mzungumzi mwenza anatakikana atumie lugha ya Kiswahili pekee ili aweze kumpa mwenzake nafasi kubwa ya kufanya mazoezi ya kuzungumza. Hali hii inampa mwanafunzi anayefanya makosa ya kimofofolojia kupata ujasiri na nafasi kubwa ya kuzungumza lugha hivyo basi kupata umahiri wa kiwango cha kuu.

iv) Kutumia lugha katika miktadha mbalimbali ili kuwa na uzoefu

Mwalimu wa lugha ya pili anapaswa kumhusisha mwanafunzi wa lugha ya pili kuzungumza lugha katika miktadha mbalimbali. Anaweza kumpatia muktadha wa uzungumzi rasmi kwa mfano kusoma taarifa za habari au muktadha wa kuigiza majukumu mbalimbali. Hali hii itamsaidia mwanafunzi kutumia lugha katika urasmi unaohitajika.

Inabainika kwamba wanafunzi wengi huwaiga walimu wao katika matamshi na namna wanavyofundisha, hivyo walimu wanaoajiriwa kulifundisha somo hili wanapaswa kupewa mafunzo na wahitimu kabla ya kuruhusiwa kufundisha lugha ya Kiswahili, na kwa walimu ambao wameathirika katika matamshi yao inapendekezwa kuwepo na mafunzo ambayo yataboresha matamshi yao ili waweze kuimarisha katika lugha ya Kiswahili na wasiweze kuhamisha matatizo yao kwa wanafunzi wa Kiswahili. Mbali na uandishi wa insha, wanafunzi wa lugha ya pili wanahimizwa kushiriki mijadala mbalimbali ili waweze kuimarika katika mazungumzo na waepuke makosa ya kimatamshi na waweze kuinua ufanisi wao wa kujifunza lugha ya pili ambayo ni Kiswahili.

1.5 HITIMISHO

Makala haya yameangazia makosa mbalimbali ya kimofofonolojia ambayo wanafunzi wenye asili ya Kitachoni walifanya katika maandishi ya insha zao na matamshi yao walipozisoma insha hizo. Makosa ambayo yalijitokeza kwa wingi katika insha za wanafunzi yalikuwa yanadhihirisha mchakato wa uchopekaji na ubadilishaji wa fonimu. Kutokana na michakato ya kimofofonolojia ambayo wanafunzi walidhihirisha katika makosa yao ya lugha ya Kiswahili kutokana na kuwa na umilisi wa lugha ya kwanza ambayo ni Kitachoni. Nadharia ya Uchanganuzi makosa iliyoasisiwa na Corder (1967) ilituongoza katika kuyachanganua makosa mbalimbali ambayo wanafunzi hawa waliyafanya. Ikumbukwe kwamba makosa mengi ambayo yalifanywa na watafitiwa ni ya kifonolojia ila yalidhihirika katika maumbo ya maneno au mofolojia na ndiposa utafiti huu ulizingatia viwango hivi viwili; fonolojia na mofolojia. Mabadiliko katika kazi andishi na za kimatamshi hutokea katika muktadha wa kimazingira wa mazungumzo na maandi maandishi. Ili kufikia kiwango cha umilisi na - utendaji wa lugha ya Kiswahili mwanafunzi anapaswa awe amekomaa katika lugha andishi na lugha zungumzi.

MAREJELEO

Corder, S. (1967) *Error Analysis:* Perspective on the second Language Acquisition. London: Longman.

Corder, S. (1981) *Error Analysis and Interlanguage*: Oxford University Press.

Habwe, J. and P Karanja. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Phoenix publishers Ltd, Nairobi.

Hooper, J. B. (1976). *An introduction to natural generative phonology.* Academic Press

Mwangi, I. (2010) *The Structure of Kiswahili: Sounds, Sound Changes and Words.* Nairobi: Focus publishers

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.